# MWIGO
# KISWAHILI
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
# KARATASI YA 2

**1. USHAIRI: SAUTI YA DHIKI**

**Mwongozo wa kusahihisha**

A. Watiliye pamba

i. Bahari (1 x 2)
Tamthilia
Sakarani – vipande viwili ukwapi na utao
- Vina 6 – 6 jumla 18 katika kila ubeti

ii. Muundo (1 x 4)
- Mishororo mitatu katika kila ubeti
- Kila mshororo una vipande viwili ukwapi na utao
- Shairi halina kibwagizo lina kiitikio
- Shairi lina jumla beti 5

iii. (1 x 4)
a) Watampoteza
b) Watakuchekelea
c) Hawataki tuwe pamoja
d) Watakutia makosa mengi
e) Watafanya tufarakane
f) Watafanya tutengene tisizikane

iv. Takriri – ituze – ituzane
Inkisari – ituze – itulize
Kufinyanga sarufi – akili ituzane
Kikae – tusifarikane – tusifarakane

v. Mipango mibaya wanayo kila kukicha na watatukosanisha

(B) Nakukumbuka

i. Tamlitha, lina mishororo mitatu katika kila ubeti

ii. Mishororo mitatu katika kila ubeti (1 x 4)
Vipande viwili – ukwapi na utao
Ukwapi mrefu na utao mfupi
Mizani 8 – 5 jumla 13
Vina ni wa ka, wa ngu, wa li (keketo) mtiririko
Halina kibwagizo, lina kiitikio
Beti jumla 3

iii. Ingawa tuko mbali, nitavumilia. Tutakuja kuwa pamoja siku moja mola akitujaalia. (1 x 3)

iv. Mi – Inkisari – mimi
Tabdila – Punguwa – Pungua
Ukijuwa – ukijua
Kufinyanga sarufi

v. Mwombe mungu uhai na uzima

2. **TAMTHILIA**
**Jeff Mandila: Upepo wa Mvua**

a)

i. Askari kshindwa kudhibiti kundi ndogo la waandamanaji ilhali wamejukumika kulinda lindi nzima uk. 25
ii. Askari wa kulinda nchi kukaa bila risasi kwa bunduki uk. 25
iii. Sengo kupendekeza watoto wa Amina kupelekwa kwa shulee ya kibinafsi ilhali wameshindwa kumudu gharama ya shule ya kiserekali.
iv. Sengo kuajiri walimu wasiohitimu kwa shule yake ilhali yeye mwenyewe amehitimu.
v. Askari wa tatu kusema kuhamasisha watu kunahitaji uvumilifu ilhali yeye ndiye alianza kwa kupiga na kuumiza mtu wa kwanza.
vi. Mtu ambaye hakuhudhuria mafunzo ya askari kupata ajira kama askari wa kulinda usalama wa nchi.
vii. Askari wa tatu kujigamba anafanya kazi nzuri na kudai nyogeza ya mshahara na cheo ilhali hakuhudhuria mafunzo ya kuwa askari licha ya elimu yake duni.
viii. Pili kuchukua hongo ili asaliti mtoto wa shoga wake wa miaka mingi.
ix. Amina kwenda kwa Msa licha ya yeye kukataza Kidani kwa sababu ya uhasama wa kale.
x. Amina kutamani Kidani apelekwe nyumbani kwa badala ya kukimbizwa hospitalini.
xi. Chifu kumwambia pili kuwa anatoa huduma kwa kila mmoja bila ubaguzi ilhali miundomsingi ya Mlimani ni bora kushinda ya Bondeni.
xii. Chifu kutangazia watu kuwa kuna usalama ilhali watu wa Bondeni wanaishi kwa hofu.
xiii. Chifu kukubali kilio cha watu ni halali na wakati huo huo kuwaambia hajaelewa wanalilia nini.
xiv. Chifu wa Lindi kuwa na hofu na usalama wa askari wake alipotaka kumtuma Bondeni
xv. Pili kutoa taarifa inayokinzana na kiongozi wa nchi juu ya usalama wa Bondeni.
xvi. Askari wa tatu kuwa na wasiwasi juu ya kiwango cha usalama huko Bondeni ilhali hao ndio wanafaa kuleta usalama kote nchini.

b) i. Muktadha wa dondoo (3 x 1)

- Msemaji ni Amina
- Msemewa: Nafsi neni au uzungumzi nafsi
- Mahali: Nyumbani kwa Amina
- Tukio: Ng’ombe hataki kufungwa kamba

ii. Mbinu za uandishi

- Nidaa – Osu!
- Maswali balagha – Kwani asante ya Punda ni teke?
- Kinaya – Badala ya ng’ombe kula nyasi anazitilia samadi
- Uzungumzi nafsi – Akh, huyu ng’ombe

iii. Migogoro (7 x 1)

1. Kidani anazozana na waadi juu ya chakula
2. Watu wa Bondeni wanazozana na watu mkahawani na kuwaita punda
3. Mtu wa kwanza azozana na watu mkahawani na kuwaita punda.
4. Mtu wa kwanza azozana na wanawake walevi na wanampiga.
5. Akida anazozana na wanafunzi watundu
6. Chifu anazozana na askari wake na kuwaita wapumbavu
7. Chifu anazozana na Amina siku ya mazishi ya Mhina.

8. Chifu anazozana na waadi na kumtia nguvuni kwa siku sita.
9. Msa alizozana na Mhina
10. Msa alizozana na Amina

**3. RIWAYA**

**Pendo la Karaha**

a) Nafasi ya vijana katika Pendo la Karaha
- Ni wasomi – Kudra, Lindo, Rukia, Kassim
- Ni walevi, waathiriwa wa dawa za kulevya: Lindo, Kassim, Swalehe
- Ni wenye bidii: Rukia, Kudra Kassim
- Ni watoro: Swalehe, Kassim
- Ni wezi: Lindo, Kassim, Rukia, Kudra
- Wauzaji wa dawa za kulevya: Regina, Jannete, Lindo
- Wenye kujali: Rukia Kudra
- Watumwa: Rukia, Kudra, Almasi, Lulu, Jane, Rose
- Wenye majuto: Almasi, Rukia, Kudra
- Kunyanyaswa: Kudra, Jane, Rose
- Kutolipwa mshahara: Kudra, Almasi
- Kudhulumiwa: Jane kutobolewa jicho na mtoto wa mwajiri wake, kubaguliwa kwa ajili ya rangi
- Kufanya kazi bila kupumzika
- Kugandamizwa Saumu kwa Kudra kupigwa mara saba
- Waajibikaji: Kudra, Rukia, Kassim baada ya kubadilika
- Tanzia kama Rose na Rukia, Lindo
- Wavumilivu; Kudra
- Kudhulumiwa kimapenzi na waajiri wao:Kudra
- Kuasi masomo: Lindo na Kassim na vijana wengine.
- Wepesi wa kushawishika: Kudra, Rukia, Lindo, Kassim
- Kuwa washiriki wa dawa za kulevya
- Kuishi katika kambi za ushauri
- Kutoka udenda barabarani
- Kubaki na mabaka meusi wanakojidunga sindano za kokani
- Walioathiriwa na dawa waliwanyonga wengine ili kuwanyang’anya watu mali zao.
- Vijana wengi waliishi kuuawa ili kung’oa jinamizi la dawa za kulevya.

b) i. Muktadha
- Msemaji ni saumu
- Msemaji ni kudra
- Mahali ni massage parlour ya Fauziya
- Kiini cha usemi Kudra alikuwa amekataa kazi baada ya Saumu kumlazimisha kwenda kwa mwanamume aliyeitwa Ali kwake nyumbani na Ali kumpeana kwa mwanamume mwingine. Pia alipitia mateso mengi kama kupigwa na Saumu.
- Matokeo ya usemi Saumu alilazimika kutoa vipasi vya wasichana wengine na wakaelekea kwenye hifadhi ya wakimbizi kungoja kupata msaada wa kurudi nyumbani.

ii. Mbinu iliyotumika katika dondoo
- Maswali balagha

iii. Sifa za msemaji
- Saumu alikuwa mkali
- Alikuwa mzingatifu katika kazi ua Fauziya
- Mwenye hasira
- Alikuwa katili alimpiga Kudra makofi na viboko na kumvunja mkono.
- Alikuwa mcheshi alicheka kila mara
- Alikuwa mpyaro – alimtolea Kudra maneno yenye sumu kali
- Alikuwa mnyanyasaji – kumtemea Kudra mate usoni
- Alikuwa kibaraka wa mwafrika aliyengandamiza wafrika wenzake.
- Msiri- hakutaka watu wajue kilichotendeka pale parlour.
- Msaliti – kupeana Kudra kwenda na mwanamume aliyeitwa Ali.
- Mwenye kiburi
- Mwenye msimamo thabiti
- Mkweli – Alimwambia Kudra maagizo ya Fauziya

iv. Jamii ya Pendo la Karaha imejawa dhuluma
- Kifo cha mzee Sanga na genge la Kuklux Klan kwa kutoboa siri ya dawa za kulevya.
- Vijana walidhulumiwa kuwauzia dawa za kulevya wenyeji wao na kutolipwa kama Lindo na Kassim.
- Kifo cha Rukia kupigwa risasi na mwajiri wake.
- Zinduna aliwadhulumu vijana walioingia kwake na pesa na zilipoisha aliwarusha nje.
- Kudra kudhulumiwa na waajiri wake Amini na Nayrat kwa kukata mshahara wake, kumfanyiza kazi muda mrefu na hata kupigwa na kudhulumiwa kimapenzi na Amini.
- Rehema kudhulumu wasichana kwa kulipwa pesa kutokana na mshahara wao kama ajenti wao.
- Kudra kufanya kazi hata akiwa mgonjwa na kutojali mamake akiwa mgonjwa
- Teresa Almasi miezi sita imepita bila kupata mshahara.
- Kudra kudhulumiwa kimapenzi na Salim mwajiri wake.
- Dele kudhulumiwa na Salim kutoruhusiwa kuhudhuria mazishi ya baba yake.
- Kudra kudhulumiwa na Saumu kwa kupigwa na kulazimishwa kwenda na mwanamme Ali.
- Rose alidhulumiwa na Saumu – motto hadi akajinyonga.
- Vijana wengi walidhulumiwa kufanya kazi bila kupumzika na bila kulipwa na kudharauliwa.
- Jane alidhulumiwa kwa kutobolewa jicho na mtoto wa mwajiri wake.

4. HADITHI FUPI

**Vazi la Mhudumu**

a) Janga la Ukimwi limeathiri vijana wengi na kuleta madhara mengi”.  Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya Mzaha mzaha.
    - Uhasama katika ndoa, kati ya msimulizi na Jabeno, pia kuna mwanamume aliyekuwa akielezea msimulizi kuathiriwa kwa uhusiano kati yake na mpenzi wake aliyemwambukiza ukimwi.
    - Kulazwa hospitali kwa ajili ya kuugua kwa wagonjwa waliokuwa hospitalini na msimulizi.
    - Kutengwa kwa waathiriwa/wagonjwa na watu wazima kama mgonjwa wa kitanda cha nne alitengwa na mpenzi wake.

- Familia kuteseka kwa kutunza wagonjwa wa ukimwi kama mama aliyetunza mgonjwa wa kitanda cha nne.
- Majuto kupitia kwa mgonjwa katika kitanda cha nne.
- Kuchangia umaskini kwa kugharamia matibabu
- Kulauminiana – mgonjwa wa kitanda cha nne
- Upweke unaoletwa na rafiki kukukimbia
- Kutowajibika shughuli nyingi za familia majukumu mengi kukwama.

(zozote 5 x 3 = 15)

b) Maudhui katika Kura ya Msalani

i. Ufisadi
- Watu walipinga kumchangua James kwa hofu kuwa angesambaza mbegu mbaya ya ufisadi alizopanda babake.
- Rais kushiriki ufisadi kwa kupendelea familia yake.
- Kuhongwa kwa wapiga kura kwa pesa na kanga
- James kuwahonga wenye mashua
- Askari kujaribu kumhonga Damisi na akakataa.

(3 x 1)

ii. Usaliti
- Rais kutenda kinyume na matarajio ya wananchi na kuwakera.
- Waziri Cyrus Magufulia kushindwa kujibu swali kwa kuogopa Rais atawafuta kazi.
- Rais kuvunja Bunge ili swala la Damisi lisijibiwe.
- Mkewe Damisi kutupa kura msalani
- Matayo kushikwa bila sababu na kupelekwa korokoroni
- Damisi kunyang'anywa walinzi wakati wa kampeni kwa kumpinga mtoto wa Raisi.
- Familia ya Damisi kushambuliwa na majambazi kwa sababu ya ubunge.
- Faiza kutoandamana na mmewe kwa kampeni.
- Kauzu kusaliti familia ya mwanakombo kwa kujifanya anawasaidia ilhali yeye ndiye chanzo cha kifo chake
- Wenye mashua kuwasaliti wananchi wa kijiji cha ngata.

(3 x 1)

iii. Ukoloni mamboleo
- Rais kutumia mamlaka kujinufaisha na familia yake
- Wasichana kwenda uarabuni kufanyishwa kazi kwa malipo duni.
- Wasichana kuteswa kule uarabuni na kuuawa.
- Kuendeleza utumwa kwa kupeleka wasichana uarabuni kufanya kazi.
- Wananchi kumwogopa Rais kwa kuwa na moyo wa simba.

iv. Ukatili
- Wasichana waliopelekwa uarabuni kufanyishwa kazi zaidi ya wanyama.
- Mwanakombo kuuawa uarabuni.
- Damisis kupigwa kama nyoka korokoroni
- James kuwasili na helikopta iliyoachilia upepo mkali kuwatawanya wapiga kura.
- Kura kuendelea bila Damisi kuwepo
- Damisi kufungwa pingu.

(3 x 1)

v. Ubadhirifu
- Rais kutumia mali ya umma kiholela.
- Rais kuregesha nchi nyuma kiuchumi
- Kauzu kutumia magari ya serikali kwa kampeni
- Afisa wa polisi kutumiwa vibaya kufanya kazi kwa mapendeleo kuhakikisha mashua yasitumiwe kuvusha watu kwenda kupiga kura.

(3 x 1)

5. MBINU ZA KUFUNDISHIA

a) Msamiati utamwezesha mwanafunzi:
- Kusoma ufahamu na kuulewa
- Kujieleza ipasavyo
- Kuandika insha nzuri
- Kutunga sentensi sahihi
- Kuelewa na kufasiri maagizo k.m. katika mitihani
- Kuchambua mashairi bila tatizo
- Kutambua maana za vitawe, visawe, vinyume
- Kupata motisha ya kusoma vitabu/uraibu kwa kusoma
- Kuimarishs ubunifu wake k.m wa kuandika
- Kuondoa hofu ya kuongea/kuimarisha ukakamavu wa kuongea hadharani

(5 x 2 = 10)

b) Kamusi inadokeza:
- Maana za maneno
- Aina za maneno k.m kitenzi
- Umoja na wingi wa nomino
- Mnyambuliko wa vitenzi
- Ngeli za nomino
- Visawe/vibadala vya maneno
- Matamshi ya maneno
- Mpangilio wa maneno kialfabeti
- Methali, nahau na misemo
- Asili ya neno k.m kigeni au la kizamani
- Michoro au picha za kinachorejelewa
- Vitawe vya maneno
- Mifano ya matumizi katika sentensi
- Maendeleo ya maneno

(10 x 1 = 10)

6. a)
- Kusoma mada (NTU)
- Kujadiliana kuhusu mada
- Kujadili picha
- Kutabiri matokeo
- Kusoma (NTU)
- Kutathmini kuelewa kwa wanafunzi, k.m. kwa kuuliza maswali

- Kuhakiki utabiri
- Kuwapa wanafunzi maoni jengevu

(5 x 2 = 10)

b)

- Wanafunzi wataiga usomaji fasaha wa mwalimu
- Huwawezesha kuelewa dhana za matini andishi na maneno
- Hufafanua maarifa ya awali ya mwanafunzi
- Huwapa motisha kusoma tanzu tofauti za fasihi
- Huwawezesha kuelewa matini zenye changamoto
- Huburudisha
- Huelimisha
- Ni msingi wa shughuli nyingine k.v kuandika
- Huimarisha stadi ya kusikiliza na kuongea
- Ni fursa kwao kujifunza maneno mapya
- Hukuza ushirikiano kati ya mwalimu na mwanafunzi

(10 x 1 = 10)

7. a)

- Kujasirisha wanafunzi
- Kuimarisha stadi ya kusikiliza
- Kumwezesha kutoa maamuzi ya kimaoni juu ya masuala tofauti
- Kuimarisha msamiati
- Kupanua mawazo ya mwanafunzi/asiwe na mitazamo finyu
- Kuimarisha uwezo wa kuchuka hoja
- Kukuza ubainifu/vipawa
- Kupata hoja za kuwasilisha kimaandishi k.v. katika insha.

(5 x 1 = 5)

b)

- Kuteua mada na kuifafanua
- Kuwaanda wanafuunzi mapema
- Kupanga wanafunzi katika makundi mawili ya kuunga na kupinga mada
- Kuteua viongozi wa mjadala na kuwapa majukumu
- Mwalimu awepo kudhibiti darasa
- Mwalimu anakili makosa ili ayarekebishe baadaye
- Hoja za kuunga na kupinga ziandikwe na katibu aliyeteuliwa
- Mhakiki mwanafunzi pia anakili makosa
- Hoja zilizoandikwa zisomwe
- Mwalimu aongoze kuchuja hoja
- Upande ulioshinda utangazwe
- Tuzo zitolewe kwa walioshiriki vyema
- Hoja zilizonakiliwa zitumiwe katika uandishi wa insha ya mjadala.

(10 x 1 = 10)